



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI

Mwanhuzi, Tarehe 30 Novemba 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Msoleni Dakawa anapenda kuutafarifu umma kuwa Maadhimisho ya SIKU YA UKIMWI DUNIANI kimkoa yatafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu tarehe 01 Desemba 2022.

Dakawa amesema kuwa Mgeni Rasmi katika Maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila mwaka, atakuwa **Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dkt. Yahaya Nawanda.**

Mkurugenzi Dakawa amesema Maadhimisho hayo kwa mwaka huu yanayoongozwa na Kauli Mbiu isemayo **"Imarisha Usawa"**, yatafanyika kwenye Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mwanhuzi mjini Meatu kuanzia saa 02:00 asubuhi.

Hivyo, wananchi wote mnakaribishwa kushiriki maadhimisho hayo ambayo yataambatana na huduma mbalimbali za afya ambazo ni Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU, Huduma za Macho, Upimaji wa Saratani ya Shingo ya Uzazi kwa Akina Mama, Huduma za Tohara, Chanjo ya UVIKO 19, Chanjo ya Polio kwa Watoto wenye Umri wa chini ya miaka 5 na Uchangiaji Damu kwa hiari ambapo huduma zote hizo zinatolewa bure.

Benton J. Nollo

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI